



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS,**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA MKURANGA**

25 Septemba, 2024

**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA  
WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAMU**

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 7 (1))

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga anawatangazia wananchi wote uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya Wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambapo jumla ya shilingi **2,133,795,818.92** zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2024/25, hivyo vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika ofisi za Serikali za Kijiji zilizopo katika maeneo yenu.

**Vikundi vinavyotakiwa kuomba mkopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-**

- i. Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi wa Halmashauri.
- ii. Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali.
- iii. Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea, na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia Kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu iwapo Timu ya Menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana nae katika eneo lake. Aidha, sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine.
- iv. Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali: na
- v. Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha kikundi cha vijana kinapaswa kiwe na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (**tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika au Mtendaji wa Kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinatakiwa kuwa na viambatisho vifuatavyo:- barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Mtendaji wa Kijiji, Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo, andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo na taarifa ya akaunti ya benki.

**Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 25 Oktoba 2024**

Tangazo hili limetolewa na:-



Waziri K. Kombo  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA MKURANGA**

